ST. PETER CLAVER HIGH SCHOOL
P.O Box 2175 Dodoma, Tanzania
Tel: (+255) 0753444555; 0653 738 060;
Website; www.stpeterclaver.ac.tz Email; spclaverhs@gmail.com
To Learn To Love To Serve

Form No. 2A1

BARUA YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2022 (ADMISSION LETTER)

St. Peter Claver High School ni shule ya Kikatoliki ya Shirika la Yesu (Jesuits) yenye lengo la kuwaongoza vijana wa kike na wa kiume kuendeleza vipaji vyao, kiakili kielimu na mambo mengine kwa ajili ya kuwahudumia wengine kwa utukufu mkuu wa Mungu.

MAHALI ILIPO ST PETER CLAVER HIGH SCHOOL

Shule ipo kijiji cha Ihumwa kilomita kumi na tatu **(13 Km)** kutoka Dodoma Mjini barabara mpya ya kuingia chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

DODOSO ZA KUJIUNGA

Ndugu Mzazi/ Mlezi wa: _____
Hongera sana, Mwanao amechaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari ya St. Peter Claver. Muhula wa kwanza unaanza 10/01/2022. Pre-Form One Program inaanza tarehe 25/09/2021.

MAKARIBISHO NA MATAYARISHO YA WANAFUNZI SHULENI (PRE-FORM ONE PROGRAM)

Kutakuwa na mafunzo ya awali yaani Pre-Form One kuanzia tarehe 25/09/2021 hadi 10/12/2022 kuwapa wanafunzi nafasi ya kuelewa na kuzoea mazingira mapya ya St. Peter Claver High School na kufahamiana wao kwa wao pamoja na mpangilio mzima wa ratiba ya taaluma. Wanafunzi wote waliochaguliwa wanatarijiwa kufuata masomo haya kwani wataanza masomo ya kidato cha kwanza moja kwa moja.

USAJILI

Usajili utaanza tarehe 25/09/2021 mara baada ya matokeo kutoka. Uniform zote zitapatikana shuleni kuanzia tarehe 25/09/2021. Unaombwa kuhakikisha mtoto wako ana sare kabla ya siku ya kufungua shule.

VIAMBATANISHO MUHIMU KWA AJILI YA USAJILI

Vifuatavyo ni viambatanisho muhimu vihitajikavyo kwa kupokelewa kwa mwanafunzi.

- Barua ya kujiunga na masomo (Hii barua) 2A1
- Fomu ya Mahitaji ya Mwanafunzi 2A2, 2A3
- Fomu ya usajili uliokamilika 2B
- Cheti cha uchunguzi wa afya kutoka kwa daktari/ hospitali 2C
- Fomu ya Statement of Policy 2D
- Fomu ya Declaration 2E
- Risiti ya malipo ya ada na michango mingine.

HELA ZA USAJILI NA ADA YA PRE-FORM ONE:
Kwa wanafunzi ambao watakuwa wamechaguliwa watatakiwa kulipa gharama ya **Tsh 300,000.00** (laki tatu) kabla ya **tarehe 28 Septemba 2021** kwa ajili ya **kushika nafasi**. Pesa hiyo **HAITARUDISHWA.**

Watakao chaguliwa wahudhurie **PRE-FORM ONE, hii ni lazima kwa waliosoma shule za Kiswahili medium**, hapa shuleni kuanzia tarehe **25 September 2021 hadi tarehe 10 December 2021**. Malipo ni **Tshs 500,000.00** (laki tano) kwa kozi ya Pre-Form One**.** Mwisho wa kulipa pesa hizo ni tarehe **28 Septemba 2021.**

Fedha ya usajili na ada kwa ajili ya Pre-Form One zilipwe kupitia akaunti za shule kama zilivyoandikwa hapo chini kabla ya tarehe **28 Septemba 2021**.

JEDWALI LA MALIPO

MALIPO	JINA LA BENKI	JINA LA AKAUNTI	AKAUNTI NAMBA
ADA YA SHULE	CRDB - UDOM	PETER CLAVER HIGH SCHOOL	01J1083847900
ADA YA SHULE	NMB - UDOM	PETER CLAVER HIGH SCHOOL	52010009203
MATUMIZI/MATIBABU	CRDB - UDOM	PETER CLAVER HIGH SCHOOL	0152083847900

Izingatiwe kwamba malipo haya ya **Registration (300,000)** na **Pre-form One (500,000)** sio sehemu ya malipo ya ada, na haitarudishwa endapo mwanao hatafika. Wanafunzi waliochaguliwa wanatakiwa kuwasili shuleni Jumatatu tarehe **25/09/2021 kati ya saa mbili asubuhi na saa kumi jioni.**
Kwa pesa za matibabu na matumizi zisiwe pungufu ya **Tsh. 100,000/-** kama kutakuwa na shida ya ziada mzazi utapewa taarifa. Kumbuka kuandika majina yote ya mwanafunzi na darasa lake katika risiti ya malipo ya Benki (Bank Pay Slip).

MALIPO YA ADA MWAKA 2022
Ada italipwa kwa awamu moja au mbili kutokana na maelekekezo yatakayotolewa na uongozi wa shule. Tukumbuke kwamba shule haitapokea ***PESA TASLIMU*** kwa malipo hayo. Risiti za malipo yote ziandikwe majina kamili ya mwanafunzi na darasa lake wakati wa malipo.
Mchanganuo wa malipo ya ada ni kama ifuatavyo:

- ***JUMLA YA ADA YOTE KWA MWAKANI NI TSH 2,700,000/=***

Mchanganuo wa ulipaji utakuwa kama ifuatavyo:-

- Malipo ya awamu ya kwanza ni Tsh **1,600,000** yalipwe kabla ya Jumatatu ya tarehe **20/12/2021.**
- Malipo ya awamu ya pili Tsh**. 1,100,000** yalipwe kabla ya Jumatatu ya tarehe **27/06/2022**.

MAHITAJI YA SARE ZA SHULE

Mwanao anatakiwa kuwa na sare za shule na zinatakiwa zinunuliwe shuleni tu. Wazazi / Walezi wanatakiwa kununua sare za shule: mbili za darasani, moja ya shamba, sweta na kizibao cha shule, tracksuit pamoja na jezi kwaajili ya michezo. Sare zote zinapatikana hapa shuleni tu. Vyombo vya kulia chakula sahani, kijiko kikombe na ndoo lazima vinunuliwe duka la shule, isipokuwa godoro na chandarua tu atapatiwa bila malipo yoyote. Wanafunzi wanatakiwa kuandika majina yao katika nguo na katika vifaa vyao vyote watakavyonunua.

Muda wa Ofisi: Ofisi zitafunguliwa **J**umatatu hadi Ijumaa kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa kumi jioni.

WAJIBU

Wazazi na wanafunzi watajulishwa kwa maandishi kwa ufupi "malengo" kabla ya usajili, shule inawakaribisha au inapokea wanafunzi wote wa kike na kiume bila kujali dini lakini kwa wanafunzi wasio Wakatoliki watatakiwa kufuata taratibu na sera za dini kama ilivyoelezwa katika kitabu cha shule.

UDANGANYIFU / ONYO

Udanganyifu katika usajili na mambo ya fedha utakaofanywa na mwanafunzi, mzazi au mlezi utapelekea kubatilishwa baada ya usajili. Endapo utagundulika udanganyifu wa aina yeyote baada ya usajili, hatua kali za haraka za kisheria za mkataba huu zitachukuliwa kuhusiana na udanganyifu huo katika zoezi zima la usajili.

SIKU YA KUWASILI SHULENI KWA MWAKA 2020 NA MIPANGILIO YA MUHULA WA MASOMO

Wanafaunzi wote wanatakiwa kuwasili shuleni siku ya Jumamosi tarehe **08/01/2022.** Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **10/01/2022**. Tarehe nyingine zitafahamika kwenye mwongozo wa Kalenda ya Shule.

Karibu sana St. Peter Claver High School. Mungu ambariki mtoto wako katika masomo yake.

……

Fr. Buberwa Karongo, SJ.

Mkuu wa Shule